BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO YA WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2023/2024

## UTANGULIZI

***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza hili kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2023/2024.

***Mheshimiwa Spika,*** Aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kwanza kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Maji, Nishati na Madini kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Wizara yake kwa Mwaka huu wa fedha 2023/2024.

***Mheshimiwa Spika,*** Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Nishari na madini pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kufanikisha kumalizika kwa kazi hii ya Kamati.

***Mheshimwa Spika,*** Kwa upekee kabisa napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa busara na hekima zake kwa mashirikiano na ushauri anaoupata kutoka kwa wasaidizi wake Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuifikisha nchi yetu mpaka hapa tulipo tukiwa katika hali ya amani na mshikamano jambo ambalo tunajivunia.

***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile, pongezi za dhati kabisa ziende kwa wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wanaouonesha kwa pamoja katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu kwa muda wote, naomba sasa niwatambue wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yahya Rashid Abdulla | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hussien Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Kombo Mwinyi Shekhe | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| 8. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |

UINGIZWAJI WA FEDHA

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inaaza kutoa maoni yake kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa masikitiko ya hali ya uingizwaji wa fedha kwa Wizara hii kutoka serikalini. Kamati imelazimika kutoa masikitiko hayo kufiatia Ripoti ya Mheshimiwa wa Waziri wa Maji, Nishati na Madini kuhusiana na Upatikanaji wa Fedha za Utekelezaji wa Shughuli walizojipangia kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika hivi sasa.

***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Waziri amefanya rejea katika Kiambatanisho namba Moja katika Hotuba yake, ambayo kinafafanua kwamba katika robo tatu za Mwaka huu , Serikali imeipatia Wizara hii asilimia **29%** tu ya fedha zote zilizotengwa kwa mwaka 2022/2023. Kamati inaishauri Serikali kuiingizia fedha zote wizara hii kwa kiasi kilichoombwa na kilichotengwa ili iweze kutekeleza majukumu yake kama walivyojipangia.

## SEKTA YA MAJI

***Mheshimiwa Spika,*** Tukiangalia utekelezaji wa Wizara hii, tuanze kutazama katika Sekta ya Maji. Mhehimiwa Waziri ameripoti kwamba hali ya uzalishaji wa nishati ya maji kwa sasa hapa Zanzibar ni asilimia **67%** ambapo kiwango hicho kinatarajiwa kupanda kwa asilimia **8%** na kufikia uzalishaji wa asilimia **75%** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yangu bado haijaridhika na kasi hii ya uzalishaji wa maji iliyopo pamoja na ongezeko linalotarajiwa hapo mwakani ukizingatia tunatarajia kuzindua miradi mingi ya maji katika muda mfupi ujao.

***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na takwimu hizo za uzalishaji wa sasa na matarajio ya mwakani, matarajio ya wananchi ni kufikiwa na huduma ya maji safi na salama katika maeneo wanayoishi na sio uzalishaji.

Hivyo, tunaiomba Wizara kuhakikisha maji yanayozalishwa yanawafikia wananchi mijini na vijijini, badala ya kuendelea kujilabu kuwa na kiwango kikubwa cha uzalishaji, wakati huduma hiyo inaishia katika matangi ya kuhifadhia maji na mabomba huku kukiwa na kiwango kikubwa cha maji yanayoendelea kupotea kutokana na mivujo inayotokana na uchakavu wa mabomba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pia imeshtushwa juu ya matokeo ya tathmini ya miradi ya Maji iliyotekelezwa hapa Zanzibar kati ya mwaka 1990 hadi 2020 ili kubaini hali ya upatikanaji wa maji na kuishauri vyema serikali juu ya namna bora ya utekelezaji wa miradi ya maji inayoendelea kwa sasa na itakayokuja.

Mheshimiwa Spika, kama alivyobainisha Mheshimiwa Waziri jumla ya miradi mitano (5) ilifanyiwa tathmini na kubainika changamoto kadhaa ikiwemo kutoshirikishwa kwa wakaazi husika na watendaji wa ZAWA wakati wa utekelezaji na kupelekea kutofikiwa kwa shabaha ya miradi hiyo.

***Mheshimiwa Spika,*** Wakati Serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini ikijiandaa na ukamilishaji na utekelezaji wa Miradi mingi ya maji katika muda mfupi ujao, tunaomba kasoro kama hizo kudhibitiwa mapema ili hatimae kupata matokea hasi ya miradi hiyo.

MAKUSANYO YA ZAWA

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Maji Zanzibar iliopangiwa kukusanya jumla ya shilingi **Bilioni 7.3** lakini hadi kufikia Mwezi Machi 2023 ilifanikiwa kukusanya shilingi **Bilioni 2.3** sawa na asilimia **32%.**

Mheshimiwa Spika, Kamati inajiuliza ZAWA inauwezo gani wa kukusanya mapato hayo wakati wateja wao na wananchi walio wengi hado hawafikiwi na huduma ya uhakika ya maji safi na salama yanayozalishwa na ZAWA.

Aidha kunataarifa za kuwa ZAWA hivi sasa haina mfumo wa kutambua wateja wao wala miundo mbinu yao. Hapa Kamati inapongeza jitihada za ZAWA kwa kazi zinazoendelea za kuwaunganisha wateja wote katika mfumo pamoja na zoezi la kuhakiki taarifa zote wateja wao katika Mikoa yote ya Zanzibar.

MIRADI YA EXIM INDIA PAMOJA UVICO 19.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uhuishwaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (**EXIM – India)** ni Miongoni mwa Miradi ya Maendeleo katika sekta ya Maji. Kamati imeridhika kwa kiasi fulani na kazi za Uchimbaji wa Visima, Ujenzi wa Matangi, Ulazaji wa Mabomba, na Ulipaji wa Fidia kwa walioathirika kwa pisha Miradi hiyo. Kazi za utekelezaji wa shughuli hizo zinaripotiwa kuwa katika hatua nzuri kwani zinafikia asilimia **85- hadi 100%.**

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli kama hizo pia zinatekelezwa katika Mradi wa Uimarishaji wa Usambazaji wa Maji Zanzibar kupitia fedha za **UVICO -19** ambao nazo hatua za utekelezaji wake zinaripotiwa kutekelezwa kwa asilimia kubwa. Kamati imejengwa na matumaini makubwa kutokana na hatua kubwa za utekelezaji wa Miradi hii.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mara nyengine tena pamoja na kupongeza hatua hiyo ambayo tunategemea itaongeza uzalishaji wa maji hapa nchini, lakini tunasisitiza haja ya kuwa na tija katika miradi hiyo kwa upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi na sio kuongeza uzalishaji, kuhifadhi au kusambazaji.

Mheshimiwa Spika, Tunalazimika kusema hivyo kwani tunaamini ya kwamba ***uzalishaji wa Nishati ya maji ni kitu chengine na Upatikanaji wa Nishati hiyo kwa wananchi katika maeneo yao ni jambo jengine.***

***Mheshimiwa Spika*,** Kwa kumalizia na hoja za Kamati katika Sekta hii ya Maji, na kwa kufanya rejea kupitia Kifungu ***PN0302*** - ***Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji*** katika kitabu cha Bajeti, tumebaini kushuka kwa Bajeti kutoka shilingi ***106,703,257,000*** kwa mwaka 2022/2023 hadi shilingi **83,768,109,000** makisio ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Kamati ilihoji juu ya jambo hili ilijulishwa kwamba, kushuka huko kwa Bajeti kunatokana na kukamilika kwa Miradi ya Maji iliyokuwa ikisimamiwa mwaka jana. Aidha

Mheshimiwa Spika, Kukamilika kwa Miradi hiyo, pia tutarajie kushuka kwa makusanyo yanayotokana na Programu hii hapo mwakani.

## SEKTA YA UMEME

***Mheshimiwa Spika,*** Tukigusia katika Sekta ya Nishati ya Umeme, Kamati inapongeza juhudi za uimarishaji wa upatikanaji wa huduma ya Umeme katika vijiji vyote vya Zanzibar kwa kubadilisha nguzo mbovu, kufanya ukaguzi wa transfoma na kuongeza idadi ya wateja wapya. Aidha tunaunga mkono juhudi za kufanya ukarabati wa miundombinu ya waya wa chini ya bahari (submarine Cable) ya zamani. Kamati inaamini kwamba juhudi hizo endapo zitafanikiwa zitapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya ukatikaji na ukosefu wa huduma ya nishati ya umeme kwa wananchi wetu.

***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile Kamati yetu inaridhika na maendeleo ya Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundombinu ya Umeme Zanzibar pamoja na Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Nishati (ZESTA). Tunaamini miradi hiyo inachochea upatikanaji wa umeme wenye kukidhi mahitaji ya taifa katika hali ya ubora, salama na upatinanaji wa umeme kwa uhakika.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia inatiwa moyo kutokana na shabaha za mwakani za ZECO. Kamati tunakubaliana na azma yao ya kuendelea kuondoa changamoto katika maeneo ambayo yanapata umeme mdogo pamoja na miundombinu chakavu. Aidha tunapongeza azma yao nyengine ya kuimarisha mifumo ili kupongeza upotevu wa umeme na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato. Kamati inatarajia mafanikio makubwa endapo shabaha hizo zitafikiwa.

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR

***Mheshimiwa Spika,*** Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kuwa, kwa upande wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mamlaka hii imefanikiwa kuvuka malengo ya Ukusanyaji wa Mapato hadi kufikia asilimia **122%.**

Kamati inapongeza hatua hii na inazihimiza taasisi nyengine kuiga Mfano wa ZURA kwa upande wa ukusanyaji.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inayo taarifa kwamba ZURA imefanikiwa kudhibiti kikamilifu huduma za maji na nishati kwa kukaguwa vyanzo 43 vya maji na kubaini kwamba vilikua vimekidhi viwango vya ubora wa matumizi ya binadamu. Aidha ZURA Ilikaguwa vituo 41 vya umeme pamoja na miundombinu ya Umeme na kugundua kuwa baadhi ya miundombini hiyo ilihitaji masawazisho. Kamati inapongeza juhudi kama hizi za udhibiti wa nishati tunazotumia ili kuhakikisha ubora na usalama wake.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaungana na Mheshimiwa Waziri kuliomba Baraza lako tukufu kukubaliana na maombi ya Mheshimiwa Waziri ya kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **20,061,335,397** kwa mwaka ujao wa fedha kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati ili iweze kutekeleza vyema majukumu yake iliyojipangia ikiwemo Kuimarisha nyenzo za Udhibiti wa Maji na Nishati pamoja na Kuandaa Kanuni za miongozo ya namna ya kudhibiti maji safi, maji machafu pamoja na miongozo ya uunganishwaji wa umeme.

## SEKTA YA NISHATI NA MADINI

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo, Mipango na Majadiliano pamoja na upembezi yakinifu juu ya kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa na chanzo chake cha kuzalisha umeme ni ya muda mrefu sasa. Takriban kila Vikao vya Kamati na Wizara hii tunapojadili utekelezaji wa Wizara tumekuwa tukipewa maelezo yanayofanana lakini yasiyokuwa na maendeleo ya utekelezaji wa suala hili. Tunaiomba Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini kulikamilisha jambo hili ili kupunguza Changamoto ya umeme Mdogo hapa Zanzibar.

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mara nyengine tena Kamati inaishauri Idara kuendelea kuhuisha Maeneo yaliyovunwa rasilimali zisizorejesheka ikiwemo mashimo ya mchanga, mawe na Kokoto pamoja na kifusi na pia kudhibiti uchimbaji haramu.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati iliwahikukaguwa uhuishwaji wa maeneo ya uvunaji wa

rasilimali zisizorejesheka Wilaya ya Kaskazini B na kushuhudia maeneo kadhaa yanayohuishwa na Serikali yakiwa katika hali isiyoridhisha huko maeneo yanayosimamiwa na watu binafsi yakinawiri vizuri na kuonesha matumaini na dalili njema za kunawiri.

Tunaiomba Wizara itafute njia bora na nafuu za uhuishaji wa maeneo yaliyochimbwa kifusi, mawe na mchanga huku ikiweka Sera, Sheria na Kanuni imara za usimamizi wa Madini Zanzibar ili kupata miongozo bora ya kiutendaji katika sekta hiyo.

***Mheshimiwa Spika*,** Kamati yetu inadhani suala hili litatekelezwa na kufanikiwa kwa kiwango kikubwa ukizingatia kuna ongezeko kubwa la fedha zilizotengwa kwa ajili ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini kutoka shilingi Milioni **48,565,000** mwaka unaomalizika hadi Shilingi Bilioni **7,042,975,000** kwa mwaka ujao wa fedha.

## UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa upande wa Uendeshaji na Uratibu wa Wizara, Kamati inazitakia heri juhudi za Maandalizi ya Usimamizi na Kufanya Mapitio ya Sera, Sheria na Mipango ya Kisekta kwa mujibu wa Vipaumbele vya wizara pamoja na kuratibu na kufanya tafiti mbali mbali zenye mnasaba na Sekta za Wizara. Tunaamini shughuli hizo zikikamilia itakua ni muongozo mzuri wa utekelezaji wa wizara hii.

HITIMISHO

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa kumalizia kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha maoni kwa niaba ya Kamati na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza.

Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuyapitisha makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini ili tumuwezeshe Mheshimiwa Waziri kutekeleza Shabaha walizojipangia.

**Naomba kuwasilisha.**

……………………….

**(Mhe: Yahya Rashid Abdalla),**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**ZANZIBAR.**